

Inaanzia wapi?

Bongani Kona

Extract translated by Richard Mabala

Inaanza wapi, hii hadithi ya jinsi ulivyotokea kulala hapa ndani ya suti yako ya buluu iliyokolea. Watu wote walidhani tulikuwa mapacha. Mama yako alituvisha nguo saresare. Tofauti pekee ni kwamba za kwangu zilikuwa mekundu na za kwako zilikuwa bluu. Tulikuwa na mabega mapana yaleyale na tulifanana kwa sura; hadi umbo la taya zetu na macho ya hudhurungi iliyokolea. 'Hapana, sisi ni binamu tu', ulilazimika kuelezea. Siku moja ulimwambia Bi Saunders, mwalimu wa shule ya Jumapili kwenye Kanisa la Kikristo ya Heathfield, 'Yeye si pacha wangu. Mama yake Christopher amefariki. Shangazi Julia ni mama yangu.' Niko kwenye misa yako ya wafu na lile kanusho lako - 'Shangazi Julia ni mama yangu' - linanichoma akili. Hadithi ya yaliyotokea kati yetu - wewe, Shangazi Julia na mimi - kwenye nyumba ya Mtaa wa Mtakatifu Patrick, yaligandia kila kitu katika maisha yetu kama kioo kilichovunjika. Sasa umekufa na mimi nimebaki peke yangu na vitu vyote hivi visivyosemeka. Vipande vilivyovunjika vya mambo ya zamani, vipande vilivyopasuka vikinikatakata. Ninarudisha muda nyuma ili nikurudishie uhai.

Wahudumu wa afya wanafungua milango ya gari la wagonjwa na kukutoa juu ya machela, mwili wako ukiwa umefunikwa na shuka jeupe. Wanakutembeza hadi mjakaranda ambapo tulikukuta; miguu yako mita moja juu ya ardhi. Wanauacha mwili wako ukining'inia kwenye upepo usiotulia na kuondoka kwa gari kutoka New Haven Drug & Alcohol Rehabilitation Centre. Machozi yanakauka na kurudi machoni mwetu wakati tunafuatana kurudi kitandani na vikweukweu na mayowe yetu yanafyonzwa na kurudi ndani ya miili yetu tena.

Pingili zako za uti wa mgongo zinarudi kwa nguvu katika nafsi yao na maisha yanarejea, yakipita kwa nguvu kwenye mishipa yako. Unafungua macho yako na kunyoosha mkono ili ufungue fundo shingoni mwako. Unashuka na kuelekea kwenye nyumba ya buluu. Unaingia nyumbani kupitia jikoni na kuweka kamba ya nailoni hapa ulipoikuta mwanzoni, kwenye gereji kandokando ya lundo la magazeti ya zamani.

Saa zinapita na rangi za zambarau, okaria na chungwa za mapambazuko zinaffia mbele ya usiku. Ninalegeza mkono wangu uliozunguka shingo lako. Na sauti ya maneno yangu yasiyojali - 'Wewe daima umekuwa mwanaharamu mnyonge, toto la mama, Abraham! Sijali kabisa ukienda kujiua - yanaffia kama ukungu uliouguzwa na joto la jua.

Na sasa unakaa pale, mzima, mwenye uhai uliorejeshwa.

Nimekaa na mhisani wako, Dirk, na wenzake wa New Haven ndani ya Kanisa la Methodist huko Green Market Square. Katika picha yako waliyo nayo huko, ulikuwa hujagusa dawa za kulevya kwa miezi kumi na tatu. Ni picha ile ya wewe ukisimama gatini huko Kalk Bay. Anga liko buluu, bila mawingu na shakwe/ndege wa baharini, wako wanaruka. Ni picha ya miaka minne iliyopita.